

“Ibrahimi, Imamu wa Mataifa”

BISMILA-HIR RAHMA-NIR RAHIM

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Asalamu Aleikum!

Ibrahimi alikuwa mtu mkuu wa Mwenyezi Mungu. Aliheshimiwa sana na Mungu, tena alichaguliwa kuwa kielelezo au mfano wa kufuatwa na wengine. Yeye anaitwa “Imamu wa Mataifa” katika Kurani Tukufu. Twatamani kuyachunguza maisha ya mtu huyu mashuhuri aliyechagua kumfuata Mungu huku ukiwapo uwezekano mkubwa kwake wa kufaulu au kushindwa. Inaelezwa katika Kurani Tukufu kwamba baba yake mwenyewe alimpinga na kuna mwelekeo mkubwa sana kwamba ndugu zake wengine walimpinga pia. Kumfuata Mungu bila ya masharti kwa upande wetu kila mara kunakuwa na gharama. Mara nyingi hawatatuelewa vizuri wale watazungukao na hasa wale wa familia yetu au umma wetu. Mtu fulani anayemfuata Mungu kwa karibu sana ataangaliwa na watu kama mtu wa ajabu, kwa maana kuifuata sauti ya Mungu kwaweza kutuleta katika mgongano na hata wale wa dini yetu.

“Na (kumbukeni khabari hii:) Mola wake alipomfanyia mthani (Nabii) Ibrahim kwa amri nyingi; naye akazitimiza. Akamwambia: ‘Hakika mimi **nitakufanya Kiongozi [Imamu] wa watu (wote)**.’ (Ibrahim akasema:) ‘Je, na katika kizazi changu pia?’ Akasema: ‘Ndio lakini’ ahadi Yangu haitawafikia (waovu) madhalimu wa nafsi zao’; (itawafikia walio wazuri).” Sura 2:124 Al Baqarah

Twataka kumwanguka mara nyingine tena huyo “Imamu wa Mataifa”, kuona aliishi miaka mingapi. Tunayo picha itokayo katika Vitabu Vitakatifu Taurati na Injili ioneshavo jinsi Ibrahimi alivyoenenda katika maisha yake. Kutoka katika vyanzo hivi sisi twaweza kupata mtazamo bora kwa nini Mwenyezi Mungu alimwita Imamu, Kiongozi wa wale wamtatufatao Mwenyezi Mungu kwa moyo wao wote.

“Kwa maana nimemjua ya kwamba atawaamuru wanawe, na nyumba yake baada yake **washike njia ya BWANA, wafanye haki na hukumu**, ili kwamba BWANA naye akamtimizie Ibrahimi ahadi zake.” Taurati Mwanzo 18:19 Hata makafiri walioishi wakati wa Ibrahimi walitambua ya kuwa Mungu alikuwa pamoja naye.

“Ikawa wakati ule Abimeleki, na Fikoli mkuu wa jeshi lake, wakamwambia Ibrahimi, wakinena, Mungu yu pamoja nawe katika yote unayotenda.” Taurati Mwanzo 21:22

Je! hivi ni dhahiri kwa makafiri wa leo kujua Mungu yu pamoja nawe na yu pamoja nami? Kama makafiri hawawezi kuona hilo, je, ni kwa sababu sisi tunashindwa kuunganika na Mungu itupasavyo?

Kielelezo cha Ibrahimi

Kuna vielelezo mbalimbali katika maisha yake Ibrahimi ambavyo yatupasa kuviangalia na ambavyo sisi tungeviangalia kama mfano kwetu wa kuiga. Ibrahimi alikuwa na mtazamo wa unyenyekevu sana kuhusu yeye mwenyewe...

“Ibrahimi akajibu, akasema, Basi, nimeshika kusema na Bwana, nami ni mavumbi na majivu tu.” Taurati Mwanzo 18:27

Taurati yasema hivi juu yake, “...Ibrahimi alisikia sauti yangu, akayahifadhi maagizo yangu, na amri zangu, na hukumu zangu, na sheria zangu.” Taurati Mwanzo 26:5

Eneo moja ambalo twatamani kuliangalia lilikuwa ni eneo lile la ukarimu wa Ibrahimi. Mtindo wake wa kumrudishia Mwenyezi Mungu utajiri wake. Kama lilivyo jambo hilo hivi leo, kwa mara nyingi sana, matajiri wamekuwa hivyo kwa sababu ya kuhodhi mali, hii ndiyo maana wao ni matajiri, walakini, Ibrahimi hakuhodhi mali kwa ajili yake binafsi. Kwa ukarimu alimrudishia Mungu sehemu ya kumi ya ongezeko la mali yake. Naam, ni jambo lisilosadikika kama lilivyo, huo ndio mfano ambao hautiliwi maanani na waumini. Wanaridhika kutoa asilimia ndogo zaidi, yaani, asilimia 2 au 3 ya mapato yao, wanasema hiyo inatosha, lakini, je, Taurati yasemaje juu ya kiwango ambacho Ibrahimi alimrudishia Mungu. Wakati uliopita Mwenyezi Mungu aliwajulisha watu kupitia wale manabii wa mwanzo kile anachotarajia kupata kutoka kwa watu wake na kile anachotaka sisi tumrudishie yeye. Mfano huo uliowekwa tangu zamani ndio Ibrahimi na wengine waliufuata wakimpa Mungu kwa moyo wa hiari. Huo ndio mfano wetu pia.

“Tena **zaka** yote ya ng’ombe, au ya kondoo, kila apitaye chini ya fimbo; **sehemu ya kumi** watakuwa ni watakatifu kwa BWANA.” Mambo ya Walawi 27:32

Hapa kwa lugha isiyoweza kukosewa ambayo hakuna awaye yote awezaye kukosea, yatuambia sisi ya kwamba Bwana alitarajia kupewa “zaka” au “sehemu ya kumi”

ambayo ndiyo maana ya “zaka”. Yaendelea kusema hivi katika Taurati:

“Tena zaka yote ya nchi, kama ni mbegu ya nchi, au kama ni matunda ya nchi, ni ya BWANA; ni takatifu kwa BWANA.” Mambo ya Walawi 27:30

Tunao ushauri huo uliofuatwa na Ibrahimi muda mrefu kabla ya wakati huu. Kumbukumbu yasema kwamba Ibrahimi alitoa sehemu ya kumi au zaka kwa kuhani wa Mungu, Melkizedeki.

“Ahimidiwe Mungu Aliye juu sana, aliyewatia adui zako mikononi mwako.” Abramam [Ibrahimi] akampa fungu la kumi la vitu vyote.” Taurati Mwanzo 14:20

Tendo hilo lilikuwa la maana sana ambalo Ibrahimi alilitenda kiasi kwamba liliandikwa tena miaka mingi baadaye katika Injili. “Bali yeye [Melkizedeki]; ambaye uzazi wake haukuhesabiwa kuwa umetoka kwa hao, alitwaa sehemu ya kumi kwa Ibrahimi, akambariki yeye aliye na ile ahadi.”

Injili Waebrania 7:6

Mwenyezi Mungu auliza Swali!

“Je! mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mnaniibia mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu [sadaka].” Malaki 3:8

Hapo kale watu wake Mwenyezi Mungu walimwibia kwa kukataa kumrudishia zaka au sehemu ya kumi. Waliitumia wenyewe, na kujifanya matajiri, lakini tendo hilo lilifikiriwa kuwa ni kumwibia Mungu.

Jambo hilo lipo hata leo. Mwenyezi Mungu ametupa utajiri wake kwa wingi, naye anataka sisi tumrudishie sehemu ya kumi ya ongezeko tupatalo na juu ya hiyo tutoe sadaka. Hapo kale wale waliokuwa waaminifu katika Israeli walitoa asilimia ishirini au hata zaidi kwa ajili ya kazi ya Mungu. Leo hii sisi kama watu tuishio mwisho wa kufungwa historia ya ulimwengu huu yatupasa kulizingatia hilo kwa makini sana na kuuiga mfano huo. Je, haitupasi kuwa wacha Mungu zaidi na kuwa tayari kutoa kwa moyo kama wao walivyofanya. Kitu cho chote kilicho pungufu ya hicho kwa kweli ni wizi tena ni kuzuia kile ambacho kwa haki ni chake Mwenyezi Mungu.

Maisha ya Ibrahimi yalikuwa ya ukarimu kadiri alivyoziidi kujitahidi kuwa katika amani na Mbingu. Roho ya ukarimu ni roho ya mbinguni. Mbingu ina roho ya kutoa, na roho

“Ibrahîmu, Imamu wa Mataifa”

Sura 2:124
Al Baqarah

R. M. Harnisch

Mfululizo na .37



“BWANA atamuru baraka ije juu yako katika ghala zako, na mambo yote utakayotia mkono wako; naye atakubarikia katika nchi akupayo BWANA, Mungu wako.” Kumbukumbu la Torati 28:8

Wapenda rafiki zangu, je, mpenda Mwenyezi Mungu aamuru baraka ije juu yenu? Hivi ndivyo isemavyo na hivi ndivyo atakavyofanya kama tutatekeleza masharti... je, hivi mko tayari kutii na kumrudishia sehemu ya kumi? Basi msilogope kumwomba mibarakaa ambayo Mwenyezi Mungu ataiamuru ije juu yenu!

Je, rafiki zangu, hazina yenu iko wapi? Masihi Isa anatelezea hivi kanuni hii: “Kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako.” Injili Mathayo 6:21 Rafiki zangu, sisi tungebarikiwa endapo tungefuata mfano wa Ibrahîmu, Imamu wa Mataifa, wa kumrudishia Mwenyezi Mungu sehemu ya kumi ya ongezeko la mapato yetu.

Unabii wa wakati wa mwisho

Tamati yake kuna unabii mwingi wa zamani wa Isaya 60 ambao unawajumisha Wana wa Mashariki (Islam ya leo) katika mkao wa siku za mwisho pamoja na uhusiano wao na Mwenyezi Mungu na watu wake wale walio waamini utukfu Mwenyezi Mungu na kuutanya usonge mbele ujumbe wa siku ya mwisho kabla dunia hii haijafika mwisho wake na kabla Isa hajaraja. Mpendwa, rafiki yake Mwenyezi Mungu, anakutaka wewe utanye sehemu yako katika kazi yake ya mwisho humu duniani. “Wingi wa ngamia utakufunika, ngamia vijana wa Midiani na Efa; wote watakuja kutoka Sheba; wataleta dhahabu na uvumba; na kuzitangaza sifa za BWANA. Makundi yote ya Kedari yatakusanyika kwako, kondoo waume wa Nebayothi watakutumikia; watapanda juu ya madhabahu yangu kwa kibali, nami nitaitukuza nyumba ya utukfu wangu. Ni nani hawa warukao kama wingu, na kama njiwa waendao madirshani kwao? Hakika yake viswa vitaningojea, na merikibu za Tarshishi kwanza, ili kuleta wana wako kutoka mbali, na fedha yao na dhahabu yao pamoja nao, kwa ajili ya jina la BWANA, Mungu wako, kwa ajili yake Mtakatifu wa Israel, kwa kuwa amekutukuza wewe. Na wageni watajenga kuta zako, na watalme wao watakuhudumu; maana katika ghadhabu yangu nailikupa, lakini katika upendeleo wangu nimekurehemu.” Torati Isaya 60:6-10

www.salahallah.com

hivo inajidhiritisha sana ndani ya Masihi Isa katika katarata yake kuu kuiliko zote aliyotoa pale msalabani. Kwa ajili yetu sisi Mwenyezi Mungu alimtoa Mwanawe pekee, na Kristo, alipokwisha toa vyote aliyokuwa navyo akajitoa nafasi yake, ili mwanadamu apate kuokolewa. Kilichotendeka juu ya ule Wilima Moria miaka elfu mbili iliyopita huonesha kwa lugha isiyo na kifani kwamba Mbingu ilitao bora kabisa kwa ajili ya wanadamu ili kutukomboa na kutuilipia fidia tusikabiiwe na mauti ya milele. Tuko ilie kuu, Isa alipotoa uhai wake kwa ajili ya wanadamu wote lilingmusa kila mito wa Mwenyezi Mungu kuwa na moyo wa ukarimu. Kwa upande mwingine, roho ya uchoyo ni roho ya Ibilisi au Shetani. Kanuni inayoonekana katika maisha ya wale waipeenda dunia hii ni kupata, kupata. Hivyo wao wanatumainia kujipatia furaha na raha, lakini tunda lao walilolipanda linawaletea taabu na mauti. Mpaka hapo Mungu atakapoacha kuwabariki watoto wake ndipo nao watakapofunguliwa vifungo vya kumrudishia sehemu yake anayoda! apewe.

Mada ya Mwenyezi Mungu ya zaka yetu au sehemu yetu ya kumi

“Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkamjaribu kwa njia hivyo, asema BWANA wa majeshi; mje kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la. Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeye alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba, asema BWANA wa majeshi.” Malaki 3:10-11

Mwenyezi Mungu anataka sisi tumjaribu au tumpime. Ili sisi tuweze kufanya hivyo, ni lazima tumwamini kama yeye asemavyo. Mimi ningependekeza sana kwamba msomaji azithibitishhe ahadi hizo za Mwenyezi Mungu kuona kama ni za kweli! Mrudishie zaka au sehemu ya kumi ya ongezeko la mapato yako na kuona kama madirisha yatafunguka au miliano ya mbinguni hatitunguka kwa ajili yako! Ahadi ni kwamba hapatakuwa na nafasi ya kutosha kuwaka mibarakaa hivyo. Pia yeye anaahidi kuyalinda mali yetu na mashamba yetu yasiharibiwe. Mimi nimekwisha kumjaribu Mwenyezi Mungu katika jambo hilo, nami naweza ku sema kweli ya kuwa ninavyo vingi zaidi kuiliko niwezavyo kuvibeba! Mibarakaa yake inavizidi vile ninavyomrudishia yeye.